



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania  
Wizara ya Elimu, Sayansi  
na Teknolojia

# ELIMU Bulletin

JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na. 30 - 2023

@wizara\_elimuTanzania [wizara\\_elimuTZ](#) [www.facebook/moestvt.com](#) [www.wyestu.blogspot.com](#) [www.moe.go.tz](#) [ELIMUTZ](#)

Tunaboresha Elimu Yetu



Sera ya Elimu na Mafunzo ya  
Mwaka 2014 Toleo la 2023

## Sasa Rasmi

# WAMA

yapongezwa juhud  
za kuunga mkono  
elimu kwa usawa



- KAZI IENDELEE -

WIZARA YA ELIMU,  
SAYANSI NA TEKNOLOGIA

Sera ya Elimu na  
Mafunzo ya Mwaka  
2014 Toleo la 2023

**SASA  
RASMI**

Fuatilia mitandao yetu ya kijamii, vyombo ya  
habari na karibu utuuzile ili kufahamu.

Pokuwa Sera kuitiza  
[www.moe.go.tz](#)

Tutumie Barua Pepe:  
[tuzungumzesera@moe.go.tz](#)



# TAHARIRI

## Tuzo kwa watafiti mahiri chachu ya maendeleo endelevu

**M**aendeleo ya nchi yoyote duniani yategemea utafiti hasa unaolenga kutambua mahitaji ya jamii yake na kutoa suluhu juu ya changamoto zinazoikabili jamii husika katika nyanja mbalimbali za kijamii na kiuchumi. Mathalan serikali ya Tanzania inapotekeleza mipango mbalimbali kufikia azma ya uchumi wa vivanda, haina budi kuzingatia na kulipa kipaumbele suala la utafiti ili kuliwezeshe taifa kiuchumi.

Tunaipongeza serikali kwa kutekeleza miradi mbalimbali ili kuimrisha huduma bora kwa Watanzania, ikiwemo ya uimrishiwa ya miundombinu katika sekta ya elimu kuanzia elimu ya Awali, Msingi, Sekondari hadi elimu ya Juu, ambapo tumejhudia maendeleo na matokeo chanya yakijipambanua kwenye sekta hiyo muhimu.

Pia kongole kwa serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuanzisha utaratibu wa kutoa tuzo kwa Watafiti Mahiri waliochapisha Matokeo ya tafiti zao katika Majorida yenye hadhi ya Juu Kimataifa (High Impact Factor Journals).

Hatua ya kutambua mchango wa Watafiti katika nyanja za afya, sayansi shirikishi, sayansi asilia na hisabati ita-

ongeza hamasa, ari na morali kwa watafiti wetu ndani ya nchi, itaimarisha maendeleo ya kitaaluma na kuchochea ushindani wenyi tija kwa Watafiti pamoja na kutatta changamoto katika jamii na kuchangia maendeleo ya Taifa.

Wakati anatangaza washindi wa tuzo hizo Septemba 16 2023, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenya alisema kila chapisho lililofikia vigezo, Mtafiti alijipatia Shilingi za Kitanzania milioni 50, akasema hatua hiyo ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa mkakati wa kuongeza hamasa kwa watafiti ndani ya nchi katika maeneo ya sayansi na teknolojia.

Watafiti 47 kutoka taasisi za elimu ya Juu za Umma na Binafsi, walishinda tuzo kwa kuchapisha matokeo ya utafiti wao kwenye majorida yenye hadhi ya juu kimataifa katika maeneo ya sayansi shirikishi, sayansi asilia na hisabati.

Prof. Mkenda alisema nia ya Serikali ni kuona Watafiti wakijikita zaidi kwenye kufanya tafiti na si kufanya biashara ili wapate fedha, na kwamba inatamani kuona matokeo ya tafiti wanazofanya yakichapisha kwenye majorida makubwa duniani ili utafiti wao ujiuze kimataifa na kuawezesha kujikwamua kiuchumi.



### BODI YA UHARIRI

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa  
*Kamishna wa Elimu*

Atupele Mwambene  
*Mkurugenzi wa Sera na Mipango*

Sylvia Lupembe  
*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*

Nelly Mtema  
*Mhariri Msaidizi na Mwandishi TSN*

**Wachangiaji:**  
Oliva Kato

Elizabeth Pancras  
Ipyana Mwaipaja  
Veronica Chitunda

**Mawasiliano:**

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,  
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya - Dodoma  
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.  
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**  
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia



## Fursa na Ufadhilli wa Mafunzo >

# Tanzania yashukuru China kwa fursa na ufadhilli wanafunzi

**S**erikali ya Tanzania imeishukuru Serikali ya China kwa kutoa fursa na ku-fadhili wanafunzi zo kutoka Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) kwenda kusoma programu ya uhandisi nchini humo kupitia Kampuni ya Group Six International & Sino Tan Industrial Park.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mara baada ya kukabidhi bendera ya Tanzania kwa wanafunzi hao Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema hatua hiyo ni utekelezaji wa hati ya makubaliano ambayo ilisainiwa mapema mwezi Desemba 2022 kuhusu ushirikiano wa kutoa mafunzo kwa pamoa kati ya DIT na Chuo cha Chongqing Vocational Institute of Engineering cha nchini China.

Amesema China ni nchi iliyoendelea kutohaka na kukua kwa sayansi na teknolojia na hivyo kama nchi tunahitaji kujifunza kutoha kwao ili kuweza kuwa na ujuzi na kutoa mchango katika nchi yetu.

"Tunahitaji sana kujifunza kutoka nchi-

ni China, kuna kitabu kimoja kitakatifu kinasema tafuteni elimu hata China, kwa hiyo twende china tujifunze sayansi teknolojia na mafunzo ya amali," amesema Prof. Mkenda

Akizungumzia program ambayo wanafunzi hao wanakwenda kusoma Waziri Mkenda amesema ni ya miaka miwili ambayo itawawezesha kupata diploma ya Taasisi hiyo lakini pia miaka miwili hiyo itahesabika kama sehemu ya miaka minne ya Programu ambayo wanasoma hapa nchini.

"Kati ya miaka minne ya masomo Wanafunzi hawa tayari wameshasoma mwaka mmoja hapa DIT na kufanya mafunzo kwa vitendo kwenye Kampuni ya Group Six International & Sino Tan Industrial Park kwa miezi miwili. Hivyo watatumia miaka miwili nchini China na watarejea kumalizia mwaka mmoja hapa DIT na kupata shahada katika eneo hilo," amesema Waziri Mkenda

Na kuongeza "Programu hiyo ni muhimu kwa kuwa inaendana na maono ya Rais Samia ambayo aliwaahidi watanzania baada

ya kuingia madarakani na kulihutubia Bunge Aprili 22, 2021 kuwa anataka kuona elimu inayotolewa inakuwa elimu ujuzi ili wanaomiliza wawe wanaajirika kirahisi au kujajiri.

Waziri Mkenda amemshukuru Mwenyekiti wa Group six International & Sino Tan Industrial Park Janson Huang, Bodi ya DIT na Menejimenti kwa juhudzi za kuhakikisha wanafunzi hao wanakwenda China kusoma huku akiwataka wanafunzi hao kusoma kwa bidii ili watakoporeja wawe bora na wenye ujuzi wa kuweza kujajiri ama kuajirika na kuchangia maendeleo ya nchi.

Wakati huohuo Mkenda amesema nia ni kuhakikisha idadi ya wanafunzi wanaoenda katika programmu hiyo inaongezeka na kuhimiza wakufunzi pia kuenda kusoma huko.

Kwa upande wake Mkuu wa Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam Mhandisi Prof. Preksedis Ndomba amesema Wanafunzi hao kwenda China ni kutoka na makubaliano ambayo DIT imeingia na Chuo cha Chongqing Vocational Institute of Enginnering cha nchini humo kushirikana kwenye mafunzo na kwamba wanafunzi waliochaguliwa ni wale waliofanya vizuri katika masomo yao.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kampuni ya Group Six International & Sino Tan Industrial Park Mr Janson Huang amesema wanafunzi hao wanaokwenda China watasoma kwa miaka miwili na wakihitimu watatunukiwa diploma ya Taasisi hiyo.



Uwekezaji Elimu ya Juu >

# Kampasi ya UDSM kuanza kujengwa Lindi Disemba



**W**ananchi wa Mkoa wa Lindi wameishukuru Serikali baada ya kutangaza rasmi kuanza kwa ujenzi wa Kampasi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mapema mwezi Desemba mwaka huu katika eneo la Gongo kata ya Jamhuri mkoani humo.

Wananchi hao wasema hayo Julai 21, 2023 walipokutana na kuzungumza na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia juu ya utekelezaji wa mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) unao-fadhili ujenzi wa Kampasi hiyo.

Pia wameiomba Serikali kuhakikisha wakandarasi watakaotumika kujenga chuo hicho kuhakikisha wanatekeleza kazi hiyo kwa Weledi na kukamilisha kwa wakati ili Chuo kiweze kuanza kama iliyopangwa huku wakishukuru kushirikishwa toka hatua za awali za mradi.

Akitangaza kuanza kwa ujenzi huo, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema kujengwa kwa kampasi hiyo ni maelekezo ya Mhe. Rais kuhakikisha mikoa yote ambayo haina vyuo vikuu inajengewa kampasi za vyuo

vikuu.

"Leo nimekuja kutangaza rasmi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimekamilisha taratibu za kikanuni na kisheria za kuanzisha kampasi, kutakuwa na kampasi ya chuo hicho hapa Lindi na kitaanza na wanafunzi 360," amesema Prof. Mkenda

Ametaja mikoa mingine itakayojenge-wa kamapsi za Vyuo Vikuu kuwa ni Kagera, Mwanza, Shinyanga, Singida, Manyara, Tanga, Simiyu, Kigoma, Ruvuma, Rukwa Katavi, na Zanzibar (Institute of Marine Scince) na kwamba kampasi hizo zinajengwa na Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET).

Waziri Mkenda amevitaka Vyuo vikuu vitakavyojenga kampasi hizo kuzielekeza kwenye kutoa mafunzo ya amali lakini pia kufanya tafiti. Aidha amekipongeza Chuo Kikuu kwa kukamilisha taratibu hizo lakini pia Mkoa wa Lindi kwa kutoa ushirikiano wa kuhakikisha ujenzi wa chuo hicho unaanza.

Akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Mkuu wa wilaya ya Lindi Mhe. Shaibu Ndemanga ameishukuru Serikali kwa kuupata Mkoa wa Lindi Kampasi ya Chuo Kikuu

cha Dar es Salaam kwani ni jambo ambalo lilikuwa likisubiriwa kwa muda mrefu. Ameeleza kuwa tayari Mkoa umewezesha upatikanaji wa eneo zaidi ya ekari 492 na ameahidi kwa niaba ya Mkoa kutoa ushirikiano kuhakikisha kazi hiyo inakamilika kama iliyopangwa.

Kwa upande wake Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Mipango, Fedha na Utawala) Prof. Bernadetha Killian amesema kupitia mradi wa HEET Chuo Kikuu kimepata Dola za kimarekani milioni 47.5 kwa ajili ya kutekeleza mradi kupitia shughuli mbalimbali ikiwemo ujenzi wa kampasi mpya, kuanza na kuboresha mitaala, kusomesha wahadhi kwa kipindi cha miaka mitano ambapo amesema Kampasi ya Lindi itajikita zaidi katika masuala ya kilimo na ufugaji wa Nyuki na kuwa itakuwa na kituo Wilayani Ruangwa kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo na tafti.

Prof. Killian ameishukuru Wizara kwa kukiamini Chuo hicho kutekeleza miradi huo ikiwa ni pamoja na Serikali ya Mkoa wa Lindi kwa ushirikiano katika kuanzisha kampasi hiyo.



## Ushirikiano maendeleo ya elimu >



# Prof Nombo asisitiza ushirikiano na wadau maendeleo ya Elimu

**K**atibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo amesema msisitizo wa Serikali ni kuhakikisha mazingira ya utoaji elimu nchini yanakuwa bora na kuhamasisha ushiriki wa kila mdau kuchangia

kwenye sekta ya elimu.

Prof. Nombo amesema hayo jijini Dar es Salaam alipokutana na baadhi ya wanachama wa Mtandao wa elimu Tanzania (TENMET) na kutoa shukrani za Serikali kwa wadau wote wa naoendelea kuchangia kwenye Sekta ya elimu.

"Tunawashukuru sana kwa namna mnavyowekeza kwenye elimu, niwaombe katika utekelezaji wa majukumu yenu muyafikie maeneo ambayo hayajafikiwa badala ya kipeleka eneo moja mahitaji yanayofanana isipokuwa yanatekelezwa na wadau wawili tofauti," amesema Prof. Nombo.

Pia amewaomba wadau hao pamoja na kuwa moja ya lengo lao ni kuhakikisha elimu ya mtoto wa kike, kuangalia pia watoto wa kiume kwa kuwa kumekuwa na mdondoka wa watoto hao kwenye elimu.

Akizungumzia mageuzi ya elimu nchini Prof. Nombo amewaomba wadau kuungana na Serikali kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mtaala mpya kulingana na Sera mpya ikipishwa unafanyika kwa ubora.

"Nimeambiwa mmeshiriki katika michakato mbalimbali ya mabadiliko ambayo yanaendelea katika Sekta, ninyi ni sehemu ya mabadiliko hayo. Ukweli ni kwamba kulingana na kalenda za Serikali zitakaporuhusu na idhini tutakayopewa na Baraza la Mawaziri tunapanga kuanza utekelezaji wa mtaala mpya mwaka 2024 tumetenga sehemu ya bajeti kwa ajili ya kuanza utekelezaji huo lakini bado tunahitaji wadau wengine wengi," amesema Prof. Nombo

Mratibu wa Mtandao wa Elimu Tanzania (TENMET) Ochola Wayoga amesema katika utekelezaji wa majukumu yao wataendelea kushirikiana na Serikali ili kuhakikisha elimu ya mtoto wa kitanzania inakuwa bora huku Mkrugzenji Mtendaji wa HakiElimu Dkt. John Kalaghe akisema kitendo cha kutembelewa na kiongozi huyo kimewatia moyo na kwamba wataendelea kutoa taarifa za utekelezaji kwa kazi wanazozifanya.



Pongezi kwa ushirikiano >

## Mkenda: Pongezi KCB kwa jitihada za kukwamua vijana kimafunzo

**W**aziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda ameipongeza Benki ya KCB Tanzania kwa namna inavyowezesha vijana kupata mafunzo ya Amali kuititia program ya Tujari.

Akizungumza jijini Dodoma na wawakilishi wa KCB waliofika kuzungumzia programu hiyo, Waziri Mkenda amesema jitihada zinazofanyika na Benki hiyo zinaunga mkono juhud za Serikali katika kuhakikisha vijana wanapata ujuzi.

Amesema mafunzo ya amali ni muhimu sana na kwamba vijana wana kiu kubwa ya kupata mafunzo hayo kwa kuwa yanamuandaa kijana kujajiri au kuajiriwa.

"Mnachofanya KCB kinatupa picha kubwa ya kile ambacho Rais amelekeza, kuongeza fursa ya mafunzo ya amali, tunaahidi tutafanya nanyi kazi, tunataka tushirikiane katika kuwafuatilia vi-

jana wanapomaliza mafunzo na juhudi mnazowasaidia kujajiri ili kuona mafanikio yakoje na nini tunaweza kufanya katika mitaala yetu ili kuboresha," amesema Prof. Mkenda

Profesa Mkenda amewaalika wadau wengine kuendelea kushirikiana na Serikali kuhakikisha tunawekeza kwenye elimu ili kupata nguvu kazi yenye ujuzi na kuchangia katika maendeleo ya nchi.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Prof. Carolyne Nombo ameishukuru Benki ya KCB Tanzania kwa ushirikiano ambao wameonesha kwa Serikali kwa kuwasaidia vijana kupata ujuzi.

"Niwasihii vijana ambao mtakwenda kusoma kuititia program ya Tujajiri inayotolewa na Benki ya KCB Tanzania kuwa makini na mafunzo haya kwa kuwa yatawasaidia kusimama kama kijana wa kitanzania kutengeza maisha yenu na kuwa na mchango katika maendeleo ya Taifa", amesema Prof. Nombo

Akizungumzia Programu ya Tujajiri

inayotolewa na Benki ya KCB Tanzania Mkuu wa Idara ya Masoko, Mawasiliano, Uhusiano na Maendeleo ya Jamii ya Benki hiyo Christina Manyenye amesema Program hiyo ilianza mwaka 2016 na kwamba ina lengo la kubadilisha mawazo ya kijana wa kitanzania kuacha kufikiria kuajiriwa na badala yake afikirie kujajiri.

Amesema program hii ni endelevu na kwamba inawafadhili vijana asilimia 100 ya ada, vitendea kazi, mavazi yanayotumika kwenye mafunzo kwa vitendo na kwamba baada ya kuhitimu masomo yao wanaendelea kuwafuatilia katika biashara zao kama walezi kwa kuwapa ushauri na wakati mwininge mitaji.

"Kwa mwaka huu tutawezesha mafunzo kwa vijana 5000 kuititia vyuo vya Ufundu na mafunzo ya Ufundu Stadi Tanzania Bara na Zanzibar. Baadhi ya Mikoa nufaika Tanzania bara kuwa ni Dar es Salaam, Mwanza, Arusha Morogoro Kilimanjaro na Geita," amesema Christina.



## Elimu kwa Usawa >



# Taasisi ya WAMA yapongezwa juhudzi za kuunga mkono elimu kwa usawa

**W**aziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amepongeza Taasisi ya WAMA kwa kutoa fursa ya elimu kwa watoto wanaotoka katika mazingira magumu na yatima kupitia shule ya sekondari ya Wama Nayakama iliyopo wilayani Kibiti Mkoa wa Pwani na WAMA Sharaf iliyopo Mkoani Lindi.

Waziri Mkenda ametoa pongezi hizo al-ipotembelea shule ya Wama Nakaya Kibiti kuona maendeleo ya elimu kwa shule hiyo ambapo amesema kinachofanywa na Taasisi hiyo ni kuunga mkono juhudzi za Serikali za kuhakikisha elimu bora inatolewa na kwa usawa.

"Mafanikio ninayoyaona wazi katika shule hii bila kusema ni fursa ya masomo kwa watoto hawa, pengine wasingepata

fursa ya kusoma lakini Taasisi ya WAMA inawasaidia kwa asilimia 100 na huu ndio mwelekeo wa Serikali kuhakikisha hakuna anaebaki kwenye mfumo wa elimu, sasa ni lazima tuunge mkono juhudzi hizi, tuendelee kufanya kazi na ninyi," amesema Prof. Mkenda

Amesema Rais Samia amejitahidi kuhakikisha watoto wa kitanzania wanapata elimu kwa usawa kwa kuondoa ada kuanzia elimu ya Awali hadi kidato cha sita, kuongeza mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na sasa kuleta mikopo kwenye Vyuo vya kati.

"Pamoja na hayo yote yaliyofanyika, Serikali inajitahidi kwenye mgawanyo wa rasilimali kila mahali kuna miradi ya elimu inaendelea lengo ni kuhakikisha haku na mtoto anachwa kwenye mfumo wa

elimu," ameongeza Waziri Mkenda

Amesema Serikali pamoja na kuongeza mikopo inatoa Samia Scholarship kwa wanafunzi wanaofanya vizuri sana kidato cha sita katika masomo ya sayansi na kuingia Chuo Kikuu kusoma Sayansi, Hisabati Tehema Uhandisi au Elimu tiba hivyo amewaasa wanafunzi hao kusoma kwa bidii ili kufaulu kwa alama za juu ili waweze kupata ufadili huo.

Kwa upande wake Afisa Elimu wa Taasisi ya WAMA Mohamed Zome amesema Shule hiyo ilianza mwaka 2010 na kwamba inachukua wanafunzi wanaotoka katika mazingira magumu nchi wote wakifadiliwa na Taasisi hiyo.

Amesema Shule hiyo kwa sasa ina wanafunzi 292 na inatoa michepuo yote. Akizungumzia ufaulu wa shule hiyo Zome amesema shule hiyo inafanya vizuri na kwamba katika matokeo ya kidato cha sita wanafunzi 54 wamefaulu kwa divisheni I-III kati ya wanafunzi 59 waliofanya mtihani wa Taifa wa kuhitimu kidato cha sita.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi katika shule hiyo wamefurahia ujio wa Waziri wa elimu katika shule hiyo na kuhidi kufanya vizuri katika masomo yao ili waweze kupata samia Scholarship.

TEHAMA na ufundishaji >

## Dkt Rwezimula awataka wakufunzi Chuo cha Ualimu Klerruu kuipa kipaumbele TEHAMA katika ufundishaji



N<sup>aibu</sup> Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Franklin Rwezimula amewataka Wakufunzi katika Chuo cha Ualimu Klerruu mkoani Iringa kulipa kipaumbele suala la Tehama kutohana na umuhimu wake katika Maendeleo ya elimu.

Dkt. Rwezimula ametoa rai hiyo Agosti 9, 2023 wakati akizungumza na Wakufunzi kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika Chuo hicho ambapo amesema lazima wajiandae kikamilifu kwani serikali inachukulia teknolojia kama msingi katika ufundishaji.

Aidha Dkt. Rwezimula amewaeleza Wakufunzi hao kuhusu mageuzi ya Elimu na azma ya serikali katika kutilia mkazo Mafunzo ya Amali yanayolenga kuwapatia Ujuzi vijana wa kitanzania.

"Tunafanya mapitio kwenye sera yetu ya elimu pamoja na mitaala nyie ndio chungu cha kupikia, kwa sababu mnaenda kutekeleza hiyo mitaala. Kwenye hii sera yetu na mitaala tunasisitiza masuala ya tehma, kitu muhimu cha kuwasitisiza sasa ni suala la kujiendeleza".

"Sio lazima uende darasa, siku hizi elimu imerahisishwa, kwa kutumia Teknolojia Mwalimu unaweza kupata \*material\* kwa ajili ya kufundishia" alisema Dkt. Rwezimula.

Ameongeza kuwa katika mwelekeo huo, masomo mengi yatapewa kipaumbele kufundishwa kujenga umahiri, masomo hayo ni pamoja na kilimo, michezo na elimu ya biashara somo ambalo litafundisha misingi ya biashara ili kuwasaidia vijana kujajiri.

"Tunataka tuwafundishe vijana wetu tangu wakiwa shule ya msingi ili wanapoijajiri wawe na maarifa ya kutosha ya kusimamia miradi na biashara zao wenye na kupunguza hali ya utege-mezi" Alibainisha Dkt. Rwezimula.

Awali katika taarifa yake Mkuu wa Chuo cha Ualimu Klerruu amesema Chuo hicho kinatoa mafunzo ya Ualimu kwa kozi ya Stashahada Maalum ya Ualimu wa Sekondari, kwa wale wahitimu wa kidato cha Nne ambao wana ufaulu katika masomo ya sayansi na Stashahada ya Ualimu wa sekondari kwa wahitimu wa kidato cha Sita.

## Uwekezaji katika Sayansi >



# Prof. Mkenda asisitiza uwekezaji katika Sayansi na Teknolojia

**W**aziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amekitaka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kuwekeza kwenye Sayansi na Teknolojia ili kuchangia katika kuinua uchumi.

Prof. Mkenda ametoa rai hiyo Agosti 7, 2023 wakati akizungumza na Viongozi na Wafanyakazi wa Chuo hicho baada ya kutembelea na kujionea Maendeleo ya miradi mbalimbali inayotekelzeza na MUST.

Prof. Mkenda ameelleza kuwa kazi ya Chuo Kikuu ni kuzalisha na kusamba za maarifa, kusaka uelewa wa mambo kupitia tafiti, hivyo amesitisiza suala la uwekezaji ili kukiwesheza Chuo hicho kujipambanua vema katika dhana ya kufanya tafiti na gunduzi za Sayansi na kufundi-

sha masomo katika maeneo hayo.

"Tunahitaji kuwekeza lakini katika eneo hili sababu uwezo wetu wa Teknolojia ni duni, nchi yetu na Afrika kwa ujumla zipo nyuma kwenye maeneo ya Sayansi na Teknolojia. Hivyo tunapaswa kuwekeza zaidi ili tuweze kuinua nchi kuwa na teknolojia na zitakazo chochea uchumi" alisema Prof. Mkenda.

Ameongeza kuwa serikali itaendelea kuwasaidia wataalam na watafiti wanaozalisha maarifa katika sayansi na teknolojia na kuchapisha matokeo ya tafiti hizo katika majarida makubwa duniani, ili kuhamasisha na kuleta ushindani katika nyanja hizo muhimu kwa Maendeleo ya kiuchumi.

Nae Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) Prof. Aloys Mvuma amesema kwa kutam-

bua azma ya serikali katika kuboresha Elimu ya Amali, Chuo kimeanzisha Mitaala katika Elimu ya Ufundji, na sasa ina mitaala minne, inayotarajia kutoa Walimu mahiri wenye utaalam wa Uhandisi kwa ajili ya kufundisha Vyuo vya VETA na vile vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs).

Prof. Mvuma ameelleza kwamba MUST inajivunia kulea na kuatamia mawazo ya kibunifu yanayovumbuliwa na Wanafunzi, kwani mpaka sasa wanafunzi wanaomaliza hapo wameanzisha kampuni 19 ambazo zimeweza kutoa ajira kwa vijana.

Pamoja na hayo amefafanua kuwa "moja ya mafanikio ni Ubunifu na uten-genezaji wa mita za maji za kidijitali, zaidi ya mita 38 zimefungwa sehemu mbalimbali kwa majaribio na matokeo yake ni mazuri" alibainisha Prof. Mvuma.



## Matokeo Tuzo za Watafiti Wacahapishaji >



**W**izara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imetangaza watafiti 47 kutoka taasisi za elimu ya juu za umma na binafsi, ambao wameshinda tuzo kwa kuchapisha matokeo ya utafiti waliofanya kwenye majarida yenye hadhi ya juu kimataifa katika nyanja za afya, sayansi shirikishi, sayansi asilia na hisabati.

Akizungumza leo jijini Dodoma katika hafla ya kutangaza washindi hao, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema kila chapisho liliolofikia vigezo, mhusika atapata Sh50 milioni, ikiwa ni utekelezaji wa mkakati wa kuongeza hamasa na morali kwa watafiti katika maeneo ya sayansi na teknolojia.

"Kila chapisho lilioloshinda limetengenewa Sh50 milioni. Tunataka wahadhiri wetu wawekeze muda, akili na nguvu katika kufanya tafiti ambazo zitatatua changamoto katika jamii na kuchangia maendeleo ya Taifa," amesema Prof. Mkenda na kuongenza:

"Serikali inaona haja ya kuwawezesha wanasyansi wetu katika utafiti; tunachokifanya ni kidogo lakini kinatuma salamu. Tunataka mtafiti aweze kuchuma mai-sha yake kutohana na utafiti."

Amesema fedha walizopata zitachagiza-wa wengine kujikita kwenye utafiti wenye tija kwa Taifa na hatimaye kujikwamua ki-

## Wizara ya Elimu yatangaza washindi wa Tuzo za Watafiti waliochapisha katika majarida ya Hadhi ya Juu Kimataifa

uchumi.

"Tunataka watafiti wajikite kwenye utafiti na si kufanya biasara ili wapate fedha. Tunataka waende kwenye majarida hayo, ili utafiti wao ujiuze kimataifa na kuwezesha kujikwamua kiuchumi," amesema Prof. Mkenda.

Wakati huohuo, Waziri amezindua awamu ya pili ya uwasilishaji wa machapisho yaliyochapishwa kati ya Julai Misi 2022 na Mei 31, 2023 katika nyanja za sayansi ya kilimo na mifugo, uhandisi na Tehama. Alitaja tarehe ya mwisho kuwasilisha machapisho hayo ni Oktoba 31, 2023.

"Katika mwaka wa fedha 2022/23, ba-

jeti iliyopitishwa ilikuwa Sh1 bilioni, sasa tumetumia Sh 500 milioni katika nyanja za afya, sayansi shirikishi, sayansi asilia na hisabati. Tunafungua tena dirisha ili kuchukua nyanja tulizoacha ambazo machapisho yake yamo ndani ya kipindi hicho," amesema.

Amesema kwa wale ambao machapisho yao yalianza kuchapishwa Juni Misi 2023, dirisha hilo litatangazwa baadaye.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa kamati ya tathmini ya machapisho hayo, Prof. Yunus Mgaya kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, amesema machapisho 82 yalipokelewa na kamati hiyo kutoka kwa watafiti wa taasisi za elimu ya juu za umma na binafsi, kwenye maeneo ya afya, sayansi shirikishi, sayansi asilia na hisabati.

"Baada ya mchakato kukamilika, machapisho zo ambayo kati yake 10 ni mkondo wa sayansi asilia na hisabati na 10 kutoka mkondo wa afya ya sayansi tiba, tulibaini yamekidhi vigezo vyaa kupata tuzo," amesema. Alibainisha kuwa ndani ya machapisho hayo kuna Watanzania 47 ambao wamekidhi kupata tuzo hizo zinazogharimu Sh 500 milioni.

Hata hivyo, alisema kamati hiyo imesisitiza katika tuzo zizajo, waombaji wa-hakikishe wanawasilisha wasifu binafsi na barua za uthibitisho kutoka taasisi wanazofanyi kazi.



Mabadiliko chanya katika Elimu >

## Miongozo minne kuleta mabadiliko chanya mionganoni mwa wadau elimu - Mkenda

**W**azira ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda, amezindua miongozo minne ya elimu maalum na jumuishi ambayo inalenga kuboresha utoaji wa elimu kwa watoto wenyewe mahitaji maalum.

Miongozo hiyo ni pamoja na mwongozo wa shule ya nyumbani, ziara ya nyumbani, upimaji na ubainishaji na uendeshaji wa elimu maalum na jumuishi.

Akizindua miongozo hiyo Septemba 12, 2023 jijini Dodoma, Prof. Mkenda amesema miongozo hiyo italeta mabadiliko chanya mionganoni mwa wadau katika kutimiza azma ya Serikali ya kuwapatia furasa ya elimu bora wanafunzi wenyewe mahitaji maalum nchini.

Ametoa wito kwa viongozi, wakuu wa Taasisi na wadau wanaojishughulisha na utoaji elimu maalum na jumuishi kuendelea kushirikiana na serikali kuhamasisha umuhimu wa elimu kwa watoto wenyewe mahitaji maalum.

"Natoa rai kwa familia na wadau wa maendeleo waendelee kuona umuhimu wa kuchangia juhudzi za Serikali katika kuwapatia huduma stahiki wanafunzi wenyewe

mahitaji maalum ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika mchakato mzima wa ujifunzaji," amesema Prof. Mkenda

Amehimiza wazazi kuona umuhimu wa kuandikisha watoto wote wenyewe mahitaji maalum katika shule kwa kuzingatia mahitaji ya mtoto.

"Kwa wale watakao hitaji huduma hii ipelekwe majumbani basi wawasiliante na sisi ili kuangalia namna tutakavyowenza kufikisha huduma hii nyumbani kwa mtoto," amesema.

Aidha, amesema katika Rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 toleo la 2023 somo la elimu jumuishi na lugha ya alama litakuwa ni lazima kwa mtu yeyote anayeandalila kuwa mwalimu hapa nchini.

"Jitihada hizi kubwa mnazoziona zinatokana na msimamo wa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan na nyie wote mnajua ni mashahidi maandalizi haya yalianza mapema na kama mnavyofahamu Rais wetu anataka kuhakikisha kila mtoto anayewatala kuwa mwalimu hapa nchini.

Prof. Mkenda ameushukuru Mfuko wa Serikali ya watu wa Uingereza (UKAID) kuitia program ya Shule Bora na Ali

Kimara Foundation kwa kuchangia uandaaji na uchapishaji wa miongozo hiyo.

Akizungumza katika hafla hiyo Kamishna wa Elimu Dkt. Lyabwene Mtahabwa amesema maendeleo yoyote duniani yanaletwa na elimu na kwamba elimu bora inategemea walibu wa nyumbani ambao ni wazazi na walezi, shulen na mazingira hivyo miongozo iliyozinduliwa inalenga itasaidia katika maeneo hayo. Awali, Mkurugenzi wa Elimu maalum wa Wizara hiyo, Dkt. Magreth Matonya amefanua kuwa mwongozo wa shule ya nyumbani utasaidia kuhakikisha haachi nyuma mtoto yeyote kwenye upataji elimu.

Amesema mwongozo wa ziara ya nyumbani unakwenda kuwasaidia walimu wanaokwenda ziara za nyumbani kupata taarifa zitakazowezesha kuchukua hatua stahiki.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Awali na Msingi kutoka TAMISEMI Mwalimu Susana Nussu, amesema TAMISEMI ipo tayari kuendelea kusimamia na kutekeleza miongozo inayotolewa ya elimu maalum na jumuishi na kuhakikisha kwamba watoto wote wenyewe mahitaji maalum wanasmamiwa na wanapata elimu na afua stahiki.

Kadhalika, Mzazi wa Ali Kimara ambaye mtoto mwenye ugonjwa adimu, Sharifa Mbarak, ameshukuru Serikali kwa kuzindua miongozo hiyo na kwamba ni hatua kubwa zilizopigwa na taifa katika utoaji elimu stahiki kwa wanafunzi wenyewe mahitaji maalum.



# NUKUU > TUTAJIELEKEZA KATIKA KUFANYA MAPITIO YA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014 NA KUFANYA MAREKEBISHO KWENYE MITAALA ILIYOPO ILI IELEKEZWE KWENYE KUTOA ELIMU UJUZI KULINGANA NA MAZINGIRA YA NCHI NA SOKO LA AJIRA ,



**– Mhe. Samia Suluhu Hassan,  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania  
Bungeni - April, 2021**

## Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,  
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**  
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,  
S.L.P 6562,  
7 Mtaa wa Magogoni,  
11479 DAR ES SALAAM.  
Simu: +255 22 2113694, 2113691  
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

Mkurugenzi Mtendaji,  
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**  
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,  
Barabara ya Mandela,  
P.O. Box 76068,  
15471 DAR ES SALAAM.  
Simu: +255 736 665 533 / 739 665 533  
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

Katibu mtendaji,  
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**  
Eneo la Viwanda Mikocheni,  
Barabara ya Bagamoyo,  
S.L.P 2624 au 32019,  
14112 DAR ES SALAAM.  
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423  
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

Mtendaji Mkuu,  
**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundji (NACTVET),**  
S.L.P 17007, DODOMA.  
Simu: +255 26 2323 121 / 0733 77 77 51  
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

Mtendaji Mkuu,  
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**  
Nunge Street, Old Catholic Church Road,  
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.  
Simu: +255 23 244 0216  
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

Mkurugenzi Mkuu,  
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**  
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,  
S.L.P. 4302,  
14113 Kitonyama,  
DAR ES SALAAM.  
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749  
Baruapepe: dg@costech.or.tz

Mkurugenzi Mkuu,  
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**  
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi  
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.  
Simu: +255 0735 041168  
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

Mkurugenzi Mkuu,  
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**  
S.L.P 34578,  
Mikocheni B, Bima Road,  
DAR ES SALAAM.  
Simu:  
Barua Pepe: info@tea.or.tz  
dgt@tea.or.tz

Mkurugenzi Mkuu  
**VETA Makao Makuu,**  
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)  
Barabara ya VETA,  
S.L.P 802,  
26 DODOMA.  
Simu: +255 26 2963661  
Baruapepe: info@veta.go.tz

Mtendaji Mkuu,  
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**  
S.L.P 743,  
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,  
ARUSHA  
Simu: +255 272 9700054  
Barua Pepe: dg@taec.go.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,  
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**  
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,  
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu  
16103 Dar es Salaam  
Simu: +255 22410700  
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,  
**Ardhi University (ARU),**  
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,  
University Road,  
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.  
Simu: +255 738 357 310-12  
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,  
**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),**  
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,  
Upanga Magharibi,  
S.L.P. 65001,  
11103 DAR ES SALAAM.  
Simu: +255 22 2150302-6  
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,  
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**  
S.L.P 3000,  
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,  
01 MOROGORO  
Simu: +255 23 260511-4  
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,  
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**  
S.L.P 1, MOROGORO  
Simu:  
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz  
info@mzumbe.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,  
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**  
S.L.P 259,  
Mtaa wa Benjamin Mkapa,  
Jengo la Benjamin Mkapa,  
41107 DODOMA.  
Simu: +255 26 2310001/2/3  
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz  
relations@udom.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,  
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**  
S.L.P. 23409,  
14110 Open University Road,  
Kinondoni Municipality,  
DAR ES SALAAM  
Simu: +255 22 2668820/ 2668992  
Baruapepe: vco@out.ac.tz

RASI wa Chuo,  
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**  
Taifa Road Next to Benjamin William,  
S.L.P 2329,  
15105 DAR ES SALAAM.  
Simu: +255 22 2850975  
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz  
dpacademic@duce.ac.tz

Mkuu wa Chuo,  
**Chuo cha Ushirika Moshi,**  
06 Barabara ya Sokoine Moshi,  
S.L.P 474  
KILIMANJARO  
Simu: +255 272 751 833  
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

Mkuu wa Chuo,  
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**  
Mtaa wa Mkwawa Chuo,  
S.L.P. 2513,  
51111 IRINGA CBD.  
Simu: +255 26 2702 751  
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,  
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**  
S.L.P. 131,  
Barabara ya 01 MUST,  
01 MBEYA.  
Simu: +255 (0)25 2957542/4  
Barua pepe: vcm@mustnet.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,  
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**  
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,  
S.L.P. 447,  
23301 TENTERU, ARUSHA  
Simu +255 272970001  
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,  
**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,**  
S.L.P 976, Butiama, MARA  
Simu:  
Barua Pepe: info@mjuuat.ac.tz

Mkurugenzi  
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**  
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,  
S.L.P 9283  
DAR ES SALAAM  
Simu: +255 22 2150048/9  
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

Katibu Mtendaji,  
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**  
7 Magogoni Street,  
P.O. Box 20384,  
11479 DAR ES SALAAM  
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292  
Baruapepe: info@natcom.go.tz

Mkurugenzi,  
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW),**  
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,  
S.L.P. 20679,  
11103 DAR ES SALAAM  
Simu:  
Baruapepe: info@iae.ac.tz

Mkuu wa Chuo,  
**Chuo cha Ufundji Arusha (ATC),**  
junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,  
P.O. Box 296,  
23105 ARUSHA.  
Simu: +255 (0) 27-297 0056  
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

Mkurugenzi,  
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**  
S.L.P 1733,  
MOROGORO.

Mkuu wa Chuo,  
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**  
Kona ya Bibi Titi ya Barabara ya Morogoro  
S.L.P 2958  
11104 DAR ES SALAAM  
Simu:  
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

Mkuu wa Chuo,  
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**  
30 Barabara ya Kibada,  
S.L.P 9193,  
17107 Kigamboni,  
DAR ES SALAAM.  
Simu:  
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz

